

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI KILICHOKETI KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE.....1.12.2021.**

**WAJUMBE WA KAMATI YA FEDHA NA UONGOZI**

NA	JINA LA MJUMBE	WADHIFA	UWAKILISHI
1	Mhe.Noel Hanura Buliho	Mwenyekiti H/Mji-Kasulu	Mwenyekiti
2	Dollar Rajabu Kusenge	Mkurugenzi Halmashauri ya Mji	Katibu
3	Mhe.Seleman Jonas Kwirusha	Makamu Mwenyekiti H/Mji	Mjumbe
4	Mhe. Ezron Budulege	Diwani kata ya Muganza	Mjumbe
5	Mhe.Ayubu Ngalaba	Diwani Kata ya Kigondo	Mjumbe
6	Mhe.Shagwe Yohana	Diwani Viti-Maalum	Mjumbe
7	Mhe: Emmanuel Gamuye	Diwani kata ya Mwilamvya	Mjumbe

**WAJUMBE WASIOHUDHURIA**

NA	JINA LA MJUMBE	WADHIFA	UWAKILISHI
1	Mhe.Prof. Joyce L. Ndalichako	Mbunge wa Jimbo la Kasulu Mjini	Kwa-Taarifa

**WAKUU WA IDARA**

NA	JINA LA MJUMBE	WADHIFA
1	Asia Matitu	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
2	Pascalina Mabena	Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
3	Godfrey Ntembeje	Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
4	Edwin Rwekaza	Mwanasheria
5	Eng.Mhamed Mwaduga	K/Mkuu wa Idara ya Ujenzi
6	Felix Mkirya	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
7	Julius Buberwa	Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
8	Halima Abubakary	Mkuu wa Idara ya Kilimo na Ushirika
9	Joseph Nsana	K/Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
10	Pesha Mwesiga	K/Mkuu wa Idara ya Ardhi na Mipango Miji
11	Casmir Charles	Kaimu Mkuu wa Idara ya Mipango na Ufuatiliaji
12	Timotheo Mathayo	Afisa Habari na Uhusiano
13	Dr, Sudi Kundelya	Mkuu wa Idara ya Mifugo na uvuvi
14	Daudi Sichinga	Afisa Michezo
15	Hassan J. Lucas	Afisa Tarafa Heru chini

16	Kyamani Kaijage	Mwandishi wa Vikao
17	Sospiter Alphonce	K/Mkuu wa Kitengo cha Tehama
18	Joseph Bisura	Afisa Mazingira
19	Felix Mkirya	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
20	Sabato A. Kgongo	Afisa Tarafaa Heru juu
21	Nurfus Aziz Ndee	Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii
22	Stephen Koberou	Afisa Biashara

### **AGENDA NAMBA 01/12/2021: -KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti alitumia fursa hii kuwakaribisha wajumbe kikaoni. Aidha aliwasihi wajumbe kuwa makini katika uchangiaji wa hoja ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti aliwathibitishia wajumbe kuwa michango na mapendekezo yao yatathaminiwa na kufanyiwa kazi ipasavyo. Baada ya kusema hayo alifungua kikao mnamo saa **4:00** za Asubuhi.

### **AGENDA NAMBA 02.12.2021: -KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO CHA TAREHE.....1.12.2021**

1. Kufungua Kikao
2. Kusoma na kuthibitisha Agenda za Kikao cha tarehe.....**1.12.2021**
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao cha tarehe.....**05.11.2021**
4. Kuwasilisha Taarifa ya Utekelezaji wa Yatokanayo na kikao cha Tarehe.....**05.11.2021**
5. Taarifa ya Mapto na Matumizi kwa kipindi cha Mwezi Oktoba.....**2021/2022**
6. Ulipaji wa fidia kata ya Mwilamvya na Nyasha
7. Maandalizi ya Wiki ya maendeleo ya Kasulu
8. Taarifa ya Ujenzi wa Madarasa ya UVIKO 19
9. Taarifa ya Mapekezi ya Fedha kwa ajii ya Miradi ya Maendeleo.
10. Utoaji wa mikopo kwa Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu.
11. Taarifa ya mwenge
12. Mengineyo
13. Kufunga Kikao.



**AGENDA NAMBA 03/12/2021: -KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 05.11. 2021**

Katibu wa kamati aliwasomea wajumbe muhtasari wa kikao cha tarehe **05.11. 2021**. Muhtasari ulipokelewa na wajumbe. Baada ya hapo ulisainiwa ili kuwa kumbukumbu sahihi ya kikao cha tarehe **05.11.2021**.

**AGENDA NAMBA 04/12/2021: - KUWASILISHA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 05.11.2021.**

Taarifa ya utekelezaji wa maagizo mbalimbali iliwasilishwa na kujadiliwa na wajumbe. Baada ya wajumbe kujadili taarifa hiyo kwa kina, walipongeza taarifa hiyo kwa utekelezaji wa maagizo mbalimbali yaliyoagizwa kwenye kikao kilichofanyika tarehe **05.11.2021**. Wajumbe waliagiza yafuatayo: -

- a) Iliagizwa kuwa Kamati ya fedha na Uongozi ifanye ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa madarasa ya **UVIKO 19** ili kuweza kuona hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inavyoendelea kutekelezwa

**AGENDA NAMBA 05/12/2021: -TAARIFA YA FEDHA KUHUSU MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI OKTOBA 2021.**

Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Mji-Kasulu kwa Mwaka wa fedha 2021/2022 ilikisia kupata jumla ya TZs.29,657,331,162.56 ikiwa ni mapato yote ya Halmashauri Pamoja na bajeti hiyo iliyopitishwa,

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilikuwa na bakaa ya fedha TZs.189,541,152.60 na kufanya jumla ya bajeti ya Halmashauri kuwa TZs 29,846,872,315.16. Aidha ilielezwa kuwa kwa kiindi cha mwezi oktoba 2021 Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilikusanya jumla ya Tsh 186,966,491.99 kati ya fedha hizo Tsh 146,452,316.99 zilikuwa mapato ya ndani yasiyo na masharti na tsh 20,514,172.63 ni mapato ya ndani yenye masharti (BIMA,CHF,USER FEES na Ada ya Shule.

Hivyo jumla ya maato yote ya ndani yasiyo na masharti kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai-Oktoba 2021/2022 inakuwa ni Tsh 579,038,347.89 sawa na asilimia ya makusanyo yote 37.5. Aidha ilielezwa kuwa Halmashauri ya Mji kwa kipindi cha mwezi oktoba pekee imepokea jumla ya Fedha Tsh 1,598,388,556.99 ikiwa ni mapato ya ndani yenye masharti na yasiyo na masharti, ruzuku za matumizi ya kwaida, mishahara na miradi ya maendeleo na kufanya jumla ya mapato kuwa Tsh 409,656,048.52

Baada ya taarifa hii kujadiliwa walishauri na kuagiza yafuatayo:

- Ilishauriwa kuwa juhudi zaidi ziongwe katika suala zima la ukusanyaji mapato licha Halmashauri kuwa kwenye hatua nzuri katika suala zima la ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri.

#### **AGENDA NAMBA 06/11/2021: TAARIFA YA ULIPAJI WA FIDIA KATA YA MWILAMVYA NA NYANSHA.**

Kaimu Afisa Mipango Miji aliwasilisha ombi la kulipa fidia eneo la mwilamvywa Pamoja eneo la Nyansha kwa ajili ya ujenzi wa shule ya Sekondari na ujenzi wa viwanda vidogo vidogo kwa upande wa Nyansha pia alieleza kuwa tayari wananchi wote wanaotakiwa kulipwa fidia wameishatambuliwa na kinachosubiriwa ni malipo tu ili sasa kazi nyingine ziweze kuendelea.

Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa suala hilo linafanyiwa kazi na wananchi hao watalipwa fidia ndani ya mwezi wa Desemba 2021 kwa ajili ya kupisha ujenzi wa Sekondari, Aidha aliwaeleza wajumbe kuwa suala hili lipo kwenye Bajeti ya 2021/2022 na utekelezaji wake utafanyika kama ilivyopangwa.

Na mara baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe waliagiza na kushauri yafuatayo; Iliagizwa kuwa suala la ulipaji wa fidia katika eneo la Mwilamvywa ni vizuri mchakato wa kulipa fidia uanze ili kuweza kudhibiti tatizo la kuchelewesha fidia na hatimaye maeneo hayo kuweza kupanda thamani. Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa kwakuwa shule ya sekondari Mwilamvywa fedha zake za ujenzi zimeshaletwa, Halmashauri kuanzia tarehe 01.12.2021 itaelekeza mapato yake yote kulipa fidia katika eneo la Mwilamvywa.

#### **AGENDA NAMBA 07/12/2021: - TAARIFA YA MAANDALIZI YA WIKI YA MAENDELEO KASULU.**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii aliwasilisha taarifa ya maandalizi ya wiki ya maendeleo kasulu, aliwajulisha wajumbe kuwa Halmashauri inategemea kuwa na wiki maalum ya maendeleo ambayo itahusisha zoezi la mbio fupi, funding Gala, kuzindua Mpango Mkakati wa Halmashauri kwa kipindi cha miaka 5, Maeneo ya uwekezaji kasudeco 1 & 2 (Yazingatiwe), Uchambuzi wa wadau, Mwami Ntale Kasulu- Marathon, Kuweka sakafu madarasa yote yasiyokuwa na sakafu, Partnership meeting, Business forum , Ujenzi wa jengo la mikutano ya Halmashauri ya Mji-Kasulu.

Mara baada ya taarifa hii kuwasilishwa wajumbe walipongeza mpango huu kuwa ni mpango mzuri ambao utaleta Maendeleo katika Mji wetu wa Kasulu pia wajumbe walisisitiza maandalizi yaendeleo kama ilivyopangwa ili kuhakikisha suala hili linatekelezwa



## **AGENDA NAMBA 08/12/2021: -TAARIFA YA UJENZI WA MADARASA YA UVIKO 19.**

Mkuu wa Idara ya Mipango na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya ujenzi wa madarasa ya UVIKO 19 na kuwaeleza kuwa Halmashauri ya Mji Kasulu ilipokea fedha kiasi cha Tsh 1,140,000,000 tarehe 21/10/2021 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 57. Fedha hizi zilipokelewa kutoka Serikali kuu kupitia chanzo cha fedha IMF na ziliingizwa moja kwa moja katika akaunti za Shule za Sekondari. Ujenzi huu umetelekezwa katika shule za Sekondari 17. Aidha aliwajulisha kuwa majengo yote yapo katika hatua za mwisho kukamilika.

Mara baada ya taarifa kuwasilishwa wajumbe walipongeza kwa jitihada kubwa zinazofanyika kuhakikisha madarasa haya yanakamilika pia wajumbe waliagiza na kushauri yafuatayo;

- Iliagizwa kuwa Kamati ya fedha na Uongozi ifanye ziara ya ukaguzi wa ujenzi wa madarasa ya **UVIKO 19** ili kuweza kuona hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo inavyoendelea kutekelezwa.
- Pia Katibu wa Kikao ambaye pia ni Mkurugenzi aliwajulisha wajumbe kuwa nguvu zaidi imeelekezwa kwenye miradi ya Ujenzi wa Madarasa katika shule za sekondari kwakuwa miradi hiyo ifikapo tarehe 15.12.2021 inatakiwa kuwa imekamilika na Waziri mwenye dhamana wa TAMISEMI atatoa ripoti dhidi ya ujenzi wa madarasa katika Halmashauri zote nchini.
- Kuhusu suala la Ujenzi wa Choo cha Walimu katika shule ya Msingi Sunzu: -Iliagizwa kuwa utaratibu ufanyike kwa shule zote zenye changamoto ya ukosefu wa vyoo vya walimu ili kuweza kuondoa adha inayowapata walimu kuendelea kuchangia choo kimoja na wanafunzi. Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa suala hili litafanyiwa kazi mara baada ya kupokea fedha za ujenzi wa vyoo kutoka UN-HABITAT pmaoja na serikali kuu ambazo zitapunguza changamoto ya ukosefu wa vyoo katika shule za Msingi.

## **AGENDA NAMBA 09/12/2021: -TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO.**

Mkuu wa Idara ya Mipango na Ufuatiliaji aliwasilisha taarifa ya mapokezi ya fedha za Miradi ya Maendeleo na kuwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Mji wa Kasulu imepokea Tsh 112,500,000. kutoka Serikali kuu kwa ajili ya ukamilishaji wa Maboma kama ilivyopangwa kwenye Bajeti ya Mwaka 2021/2022. Aidha aliwajulisha kuwa tumepokea 340,000,000/= za UVIKO 19 kwa ajili ya ujenzi wa miundo mbinu ya Afya 250,000,000 zitatumika kujenga jengo la ICU katika Hospitali ya Mji wa Kasulu,90,000,000 zitatumika kujenga nyumba za Watumishi

Pia aliwaeleza kuwa Halmashauri imepokea Tsh 126,000,000 kutoka UNFPA ambapo 56,000,00 zitatumia kujeng Maternity <sup>Wing</sup> na mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika Zahanati ya Kigondo na 35,000,000 kujenga jeno la huduma Rafiki kwa vijana katika zahanati ya Murufiti na 35,000,000 zitahamishiwa katika zahanati ya Kazuramimba.

Pia Tsh 940,000,000 zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa Sekondari mpya za Kimobwa na wilamvya kila moja Tsh 470,000,000. Aidha Halmashauri imepokea Tsh 100,000,000 kwa ujenzi wa nyumba 2 za walimu katika Sekondari Nyumbigwa kutoka TEA

Mara baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe walipongeza na kushauri kuwa utekelezaji ufanyike mara moja na pia

- Iliagizwa kuwa kufanyike ufuatiliaji wa fedha za Ujenzi wa Kituo cha Afya Heru-Juu ili kuweza kurejesha fedha hiyo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya. Mkurugenzi aliwajulisha wajumbe kuwa suala hili linaendelea kufatiliwa kwa ukaribu na fedha hiyo italetwa.

#### **AGENDA NAMBA 10/12/2021: -TAARIFA YA UTOAJI WA MIKOPO KWA WANAWAKE, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.**

Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii aliwasilisha taarifa ya utoaji wa mikopo kwa wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu na alieleza kuwa katika awamu hii vitakopeshwa vikundi 4 kati ya hivyo vijana ni vikundi 2 vitakavyo gharimu Tsh 122,000,000/+ na vikundi 2 vya Wanawake vitagharimu tsh 112,000,000 ambapo jumla ya Tsh 134,000,000/=zinakwenda kukopeshwa kwa mchanganuo ufuatao;

Tsh 63,483,699 zimetokana na mapato ya ndani kwa maana ya asilimia 10 na Tsh 70,516,301 zimetokana na marejesho ya vikundi. Mara baada ya taarifa hiyo kuwasilishwa wajumbe walishauri na kuagiza yafuatayo;

- Iliagizwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uongozi wafanye ziara ya kutembelea kikundi cha (IPOSA) ili kuweza kutazama kama uwekezaji wa kiasi cha fedha Tshs. 110,000,000/=kitaweza kurejeshwa na wajumbe waweze kukifahamu pia.
- Katibu aliwajulisha wajumbe kuwa katika awamu nyingine mapendekezo ya utoaji wa mikopo kwa vikundi yatatazama katika maeneo yote kwa kuzingatia vigezo vya utoaji wa mikopo kutoka katika kata zote za Halmashauri.

#### **AGENDA NAMBA 11/12/2021: -TAARIFA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU KWA MWAKA 2021.**

Mkuu wa kitengo cha Utamaduni Sanaa na Michezo aliwasilisha taarifa ya mbio za Mwenge wa Uhuru kwa Mwaka 2021 na ikapokelewa, Aidha ilijulishwa kuwa kimkoa Wilaya ya Kasulu tumekuwa nafasi ya nne na kitaifa tumekuwa namba 30 kati ya mikoa 32.

#### **AGENDA NAMBA 12/12/2021: -MENGINEYO**

- Mialiko ya wiki ya maendeleo ya Kasulu itolewe mapema ili kuweza kuwarahisishia wadau kushiriki katika wiki hiyo maalum ya maendeleo.



- Mtendaji wa kata katika soko la Kumsenga atazame namna ya kupunguza changamoto ya kuondosha matoroli yanayozagaa Mjini kwa kushirikiana na Afisa Mazingira ili kuweza kuweka Mji safi.
- Afisa Biashara afanye mazungumzo na wafanyabiashara waliofungiwa vibanda ili waweze kufunguliwa vibanda na wakati huo waendeleo kuwa wanalipa kodi hiyo taratibu huku wakiwa wametanguliza fedha kidogo.

### AGENDA NAMBA 12/12/2021: -KUFUNGA KIKAO

Kabla ya kuahirisha kikao, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa michango yao mizuri ya mawazo na kisha aliahirisha kikao mnamo saa 10:30 za Mchana.

#### MUHTASARI HUU UMETHIBITISHWA NA

NURFUS AZIZ

KATIBU



SAINI

NOEL H BULHO

MWENYEKITI



SAINI

MKURUGENZI WA HALMASHAURI YA MJI  
KASULU

TAREHE.....

13/01/2022  
MWENYEKITI WA HALMASHAURI  
HALMASHAURI YA MJI KASULU  
KASULU